

Urusi

Muafrika
yasaidia

28/7/63
Afrika

UNO, New York, Jumanne.

URUSI inatazamiwa ku-
unga mkono madai ya
nchi za Kiafrika katika
UNO kuwa Halmashauri
Kuu inayosimamia amani
ulimwenguni, atoe adhabu
ya ususaji ikiwa ni lazima
kwa Ureno ili kuilazimisha
itoe uhuru kwa makoloni
yake ya Afrika.

Mjumbe Mkuu wa Urusi,
Nikolai T. Fedorenko, pia ata-
tazamiwa kutoa lawama kubwa
kwa Amerika na nchi nyingine
za Umoja wa nchi za Maghari-
bi, kwa juhudi zao za kutoa
silaha kwa Ureno.

Akifungua majadiliano kati-
ka Halmashauri Kuu hiyo ya
UNO inayoshughulikia amani
ulimwenguni, Waziri wa nchi
ya Liberia, J. Rudolph Gri-
mes, kwa niaba ya nchi 32 za
Kiafrika ambazo ni wanacha-
ma wa UNO, alidai kuwa
Ureno isuswe kabisa katika
kila jambo. Akaongeza kuse-
ma kuwa ikiwa madai hayo
hayatatimizwa na UNO, basi
nchi za Kiafrika zitachukua
hatua yake.